**Noa bongo, jenga maisha yako.**

**"Kabumbu barani Afrika-si mchezo wa miguu pekee"**

**KIPINDI CHA NANE: "Kuwa ustadi kunahitaji nidhamu"**

**MWANDISHI: Chrispin Mwakideu**

**WAHARIRI: Andrea Schmidt,Thelma Mwadzaya**

**Orodha ya wahusika / kipindi cha nane:**

- Msimulizi

**ONYESHO LA KWANZA: KILINIKI YA SOKA KATIKA UWANJA WA JIJI**

- Safina (Mke,13)
- Jonathan (mume,15)
- Metogba (mume,28)
- Komora (mume,14)
- Sauti mchanganyiko za wasichana na wavulana (13+)
- Wakasa (mwenyekiti usimamizi wa soka, mume, 54)

**ONYESHO LA PILI: JIJI LA TAMBARARE**

- Mhe. Makemba. (mume,55)
- Komora (mume,14)
- Inspekta Tino (mume, 40)

**ONYESHO LA TATU: KITUO CHA POLISI JIJINI TAMBARARE**

- Safina (Mke,13)
- Chedede (mume,14)
- Shangazi Lily (mke, 33)

**ONYESHO LA NNE: NYUMA YA UWANJA WA JIJI**

- Chedede (mume,14)
- Safina (mke,13)
- Metogba (mume,28)
- Sauti mchanganyiko za wavulana na wasichana (13+)

**ONYESHO LA TANO: NYUMBA YA SHANGAZI LILY**

- Safina (mke,13)
- Aunt Lily (mke, 33)

**UTANGULIZI:**

1. **MSIMULIZI:** Salamu kem kem na karibu kwenye kipindi kingine cha Noa bongo, jenga maisha yako. Hiki ni kipindi cha nane katika makala ya kandanda barani Afrika. Katika kipindi kilichopita raisi aliwahutubia wananchi akiwa katika uwanja wa jiji ambako Metogba anasimamia mafunzo ya soka. Jonathan aliigundua njama iliyowashirikisha babake, Mbunge na Komora. Shangazi Lily, Metogba na Safina walimtembelea Chedede alipokuwa korokoroni. Hadithi hii itatupeleka wapi leo? Ili kupata majibu baki nasi hadi tamati ,katika kipindi chetu cha leo kiitwacho **"Kuwa stadi kunahitaji nidhamu"**. Nakupeleka moja kwa moja hadi uwanjani kwenye kliniki ya soka ambako Wakasa, mwenyekiti wa shirikisho la kandanda, ana matatizo....

**SCENE ONE: SOCCER CLINIC AT CITY STADIUM**

2. **SFX: VOICES OF YOUNG PEOPLE PLAYING FOOTBALL**

3. **WAKASA:** Metogba, Huwezi kuitelekeza timu hii kwa sababu rais hakukutaarifu kuwa atafika kuwahutubia wananchi. Yeye ni raisi! Ana haki ya kufanya analolitaka!

4. **METOGBA:** La! Sikubaliani na wewe, bwana Wakasa. Hata hivyo, ni mimi ndiye niliyetoa ombi kwa niaba ya vijana, si yeye wala serikali yake.

5. **WAKASA:** Naelewa ulivyohujumiwa Metogba, lakini tafadhali usivunjike moyo sasa. Wewe ndiye tegemeo la wachezaji hawa wa soka, isitoshe kiliniki hii ndiyo nafasi yao kubwa ya kufaulu maishani.

**6. METOGBA:** Sawa, nitaendelea... lakini kwa ajili ya soka tu. Nimechoshwa na tafash na mitafaruku niliyoipata tangu nilipoanza kliniki hii.

**SFX: : WHISTLE BLOWS, FOOTBALL PLAYING SOUNDS STOP**

**7. METOGBA: (KELELE)** Haya tosha! Njooni hapa, ala Komora yu wapi?

**8. ALL PLAYERS: MURMURS AND VOICES OF PLAYERS WITH HEAVY BREATHING**

**10.METOGBA:** Ketini chini. Sikilizeni, nafurahi kwamba bado muna muamko lakini hilo halitoshi. Bado tunahitaji kumchagua mchezaji bora kati yenu, kwa hiyo tumeandaa mechi ya kirafiki kati yetu na mabingwa wa soka wa mwaka jana, kilabu cha soka cha Tambarare. Baada ya mchuano huo nitamtangaza mwanasoka bora, atakayesajiliwa na timu yangu ya ng’ambo.

**SFX: HUGE APPLAUSE**

**9. METOGBA:** Mbali ya hilo, nimesikia kuwa mawakala wa kabumbu kutoka ulaya watahudhuria mechi hiyo, ni nafasi nzuri kwa kila mmoja wenu.

**10. SAFINA:** Komora yule yuaja!. Lakini mbona anayumbayumba vile ?

**11. ALL PLAYERS: HUGE LAUGHTER...**

**12. SFX: WHISTLE BLOWS**

13. **METOGBA:** Kimya! Komora unataka kuonyesha nini ?

14. **KOMORA: (sauti ya ulevi)** Aaah, usiniulize maswali ya kipuuzi !

15. **METOGBA:** umekunywa nini?

16. **KOMORA: (Intoxicated voice)** unataka kujua? Au unataka kuonja? Haha... haya chukuwa ganja, mvuto mmoja, na itakupeleka popote utakapo.

17. **ALL PLAYERS: LAUGHTER AGAIN.**

18. **METOGBA: (Angry)** Kimya! Munadhani haya ni masihara? Komora ni mmoja wetu, huyu amelewa na anatumia madawa ya kulevya na nyinyi munamcheka? Komora! Ondoka kiwanjani, tutajadili suala lako kesho, tembo litakapokutoka.

19. **JONATHAN:** Mkufunzi, **(Calmly)** Naelewa sababu gani Komora yuko hivi. Huu ndio wakati wa kuyaweka yote bayana!

20. **NARRATOR:** Kuna nasaha moja isemayo, unaweza kudanganya watu wakati fulani, lakini huwezi kuwadanganya watu wote wakati wote. Hayo ndiyo yaliyobainika kuhusu Komora baada ya Jonathan kuwaeleza wenzake na Metogba kuhusu ujumbe wa simu uliowachwa nyumbani kwao na Komora. Inspekta Tino alifahamishwa yote hayo pindi baada ya ukweli kujulikana na akaanza kumtazama kwa karibu zaidi Komora. Kesho yake basi jijini Tambarare...

**SCENE TWO: TAMBARARE CITY**

**21. SFX: WALKIE TALKIE SOUNDS**

**22. INSPEKTA TINO: (Talks into walkie talkie)** Bado ninamuona mtuhumiwa, narudia kuwa namuona mtuhumiwa, amelala mbele ya mlango wa duka... Ova. Ah, gari la mheshimiwa linakaribia...

**23. SFX: CITY AMBIENCE / CAR ENGINE COMES TO A STOP AUTOMATIC WINDOW OPENS.**

**24. MHE. MAKEMBA:** Wewe, Komora! Amka!

**25. SFX: CAR HORN HOOTED THREE TIMES**

**26. KOMORA: (Confused)** Ah? ..Oh Mheshimiwa.. ndio. umeniletea pesa zangu sio?

**27. MHE.MAKEMBA:** Shika, taslimu. sikiza kwa makini, usinipigie simu tena.

**28. INSPEKTA TINO:** Mikono juu! simama ! Tunawakamata nyote!

**29. MSIMULIZI**: Mambo yalikwenda kasi mithili ya duma awindapo swara, hata Mhe. Makemba hakukijua kilichokuwa kikiendelea. Walikamatwa wote pamoja na Komora, baadaye akakiri kuwa alimshawishi Komora kulivunja duka la Shah Electronics na kumtupia lawama Chedede. Safina na shangazi Lily walikuwa hapo kushuhudia kuachiliwa kwa Chedede.

**SCENE THREE: AT TAMBARARE POLICE STATION**

**30. SFX: CITY STREET SOUNDS**

**31. SAFINA:** Shangazi Lily, bado sijaamini! Nilifikiri haya mambo hutokea kwenye filamu pekee.

**32. SHANGAZI LILY:** Afadhali yamekwisha. Dede ameachiliwa huru na wahalifu wenyewe wamewekwa ndani.

**33. SAFINA:** Ningependa kukuuliza jambo.. wewe na Chedede..kwani?

**34. CHEDEDE: (Excited)** Hamujambo hapo !

**35. SAFINA / SHANGAZI LILY:** Dede!

**36. CHEDEDE:** Nimefurahi kuwaona, mmh..raha iliyoje kuwa nje na kuvuta hewa safi.

**37. SAFINA:** Wakati Jonathan alipotueleza kuhusu simu na njama ya babake na Komora waliopanga, sote tuliduwaa!

**38. SHANGAZI LILY:** Sawa, hebu twendeni, musije mukachelewa uwanjani...

**39. CHEDEDE: (In disbelief)** Siamini maskio yangu? Umemruhusu Safina kucheza mpira?

**40. SHANGAZI LILY:** Ndio, lakini kwa sharti moja. Safina lazima apambane

na wachezaji wa kiume ili apate nafasi katika timu ndipo ashiriki kwenye michuano ya Ulaya.

41. **SAFINA / CHEDEDE: (Both laugh)** Hahaha!

42. **CHEDEDE:** Nimetamani sana kurudi uwanjani...

43. **NARRATOR:** Nyuso za Shangazi Lily, Safina na Chedede zilijawa na furaha walipokuwa wakiondoka kwenye kituo cha polisi na kuelekea uwanjani. Walipowasili…..

**SCENE FOUR: BACK IN THE STADIUM**

44. **SFX: WHISTLE BLOWS.**

45. **METOGBA:** Haya! Tufanye mduara. Leo, kabla kuanza mazoezi ningelipenda kumkaribisha Chedede aliyerudi kwenye timu yetu.

46. **ALL PLAYERS: APPLAUSE FOLLOWED BY WILD CHEERS AND WHISTLES.**

47. **METOGBA:** Tosha, nani atatueleza tumejifunza nini kutokana na tukio la Komora?

48. **SAFINA:** Mkufunzi, nimejifunza kuwa bangi na kandanda havitangamani...

49. **ALL PLAYERS: LAUGHTER**

50. **METOGBA:** Swadakta! Mbali na kuwa mhalifu, Komora pia alikuwa na kosa la kutumia mihadarati. Wanamichezo wengi wameharibu kazi zao kwa ajili ya madawa. Nani atatupa mfano?

51. **CHEDEDE:** Diego Maradona. Niliiona filamu fupi kumhusu katika duka la Shah Electronics.

52. **METOGBA:** Ni kweli. Maradona alisifika kama vile Pele. Lakini umaarufu wake uliingia dosari ilipojulikana huko Italia kuwa anatumia madawa yakulevya aina ya Kokeini. Baadaye alipigwa marufuku kushiriki katika kombe la dunia mwaka 1994 kwasababu ya matumizi wa madawa haramu. Yote tisa, kumi ni, kuwa mchezaji kabumbu mzuri, ni lazima afanye mazoezi na awe na nidhamu. Sasa ningependa mpira huu upitishwe mikononi mwenu, muutizame kwa makini...

53. **ALL PLAYERS: MURMURS AND VOICES**

54. **METOGBA:** Sikusema muzungumze. Tosha. Nani atanieleza kuhusu mpira huo?

55. **NARRATOR:** Metogba alitumia fursa hiyo kuwaeleza wachezaji hao chipukizi kuwa, stadi wa soka analazimika kuudhibiti mpira, ila matumizi ya madawa ya kulevya na tembo yanauathiri uwezo huo. Alitilia mkazo umuhimu wa kutotumia madawa ya kulevya ili kufanikiwa michezoni. Wakati wote huu, Safina alikuwa akimuwaza shangazi yake, na alipofika nyumbani....

## SCENE FIVE: AT AUNT LILY'S

**56. SAFINA:** Shangazi Lily nikuulize kitu?

**57. SHANGAZI LILY: (Angrily)** Huwezi kuamini niliyosikia redioni. Makemba ameachiwa huru kwa dhamana, hilo ndilo tatizo la serikali yetu. Ukiwa na pesa unaweza kuzivunja sheria. Chedede hakuwa na hatia na akazuiliwa korokoroni kwa siku kadhaa. Wahalifu wameshikwa ila yeye amelipa vijipesa, kisha huyo... yu huru kama ndege angani!

**58. SAFINA: (Embarrased)** Kwa kweli inasikitisha.

**59. SHANAGZI LILY:** Ulitaka kuniuliza kitu...

**60. SAFINA: (with sense of shame)** Shangazi Lily, Leo katika kliniki ya mpira tumejifunza mengi. Metogba alizungumzia kuhusu athari za pombe na madawa katika soka. Wakati wote huu nilikuwa nikikuwaza wewe.

**61. SHANGAZI LILY:** Mimi? Kwa nini mimi Safina, mimi si mchezaji ! **(chuckles)**

**62. SAFINA:** Najua, lakini usiku ule ulikuwa chakari, kisha hii kazi ya usiku..

**63. SHANGAZI LILY: (Shocked)** Safina! Fyata mdomo wako !

**OUTRO**

**67. NARRATOR:** Swala la matumizi ya madawa ya kulevya na pombe ni la msingi katika michezo ya kulipwa. Wanamichezo wengi wamepigwa marufuku kushiriki au wamevuliwa nishani zao kwasababu ya matumizi ya madawa haramu. Safina alikuwa na haki ya kuwa na wasiwasi kwa sababu ya shangazi yake. Mpaka wa leo haijui kazi anayoifanya… vilevile Mhe. Makemba ameachiliwa huru, ana mipango gani? Kumbuka, kuna mchuano mkubwa unaokuja, matokeo yatakuwa vipi baada ya Chedede kurejea kwenye timu tena? Kwa hayo na mengine mengi kisubiri kipindi kijacho. Ukitaka tena kusikiliza kipindi hiki au chengine kilichotangulia tembelea kurasa za tovuti **www.dw world.de/lbe**. Mpaka wakati huo, kwa heri!